JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

***Unapojibu tafadhali taja:***

**Kumb. Na. KDC/L.20/22/42** 12 Juni, 2023

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imepokea kibali cha Ajira **Kumb.Na.FA.170/361/01"B"/52 cha tarehe 30 Machi, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwaajili ya kuajiri Watendaji wa Vijiji Daraja III nafasi tano (**05**) na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja II nafasi mbili (**02**).

Kutokana na Kibali hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza **nafasi 07** kwa kada tofauti kama inavyoonekana hapa chini:-

## 1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III (NAFASI 05)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

i.) Awe Mtanzania
ii.) Awe na Elimu ya Kidato cha Nne(IV) au cha Sita(VI).
iii.) Awe na cheti cha Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo: - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iv.) Awe na umri wa miaka 18 au zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka 45.

### 1.2 MAJUKUMU:

i.) Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
ii.) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na kusimamia Utawala Bora katika Kijiji.
iii.) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
iv.) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmshauri ya Kijiji.
v.) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.

vi.) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
vii.) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika kijiji.
viii.) Kusimamia ukusanyaji na kuhifadhi kumbukumbu zote za Nyaraka za Kijiji.
ix.) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
x.) Kusimamia utungaji sheria ndogo za vijiji.

**1.3 MSHAHARA**

Cheo hiki kina ngazi ya Mshahara wa **TGS B**

## 2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 02)

**2.1 SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe Mtanzania
- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita.
- Awe na cheti cha Stashahada **au NTA level 6** katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utunzaji wa Kumbukumbu, Urasimu Ramani (Cartography) au (Geoinformatics), Sheria au Kumbukumbu za Afya kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali, mwenye ujuzi wa Kompyuta.

**2.2 MAJUKUMU YA KAZI:**

*i.)* Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista *(incoming correspondence register)*
*ii.)* Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi kwenye rejesta *(outgoing correspondence register)*
*iii.)* Kusambaza majalada kwa watendaji *(action officers)*
iv.) Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa watendaji
v.) Kutafuta kumbukumbu/Nyaraka/Majalada yanayohitajika na watendaji
vi.) Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada *(racks/filing cabinets)* au mahali pengine yanapohifadhiwa
vii.) Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (*File tracking*)

**2.3 MSHAHARA**

Cheo hiki kina ngazi ya Mshahara wa **TGS C**

**MASHARTI YA JUMLA**

i.) Awe na umri wa miaka 18 au zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka 45.
ii.) Awe na afya njema, mchapakazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.
iii.) Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (**NIDA**)

iv.) Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (Passport size) iliyoandikwa jina kwa nyuma.

v.) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

vi.) Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya Kidato cha Nne (IV) na Sita (VI), cheti cha kuzaliwa, vyeti vya taaluma (Transcript na cheti) pamoja na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika. Mwombaji atakayewasilisha "**Result Slip", "Statement of Result", "Provisional Result", au "Transcript"** bila nakala halisi ya cheti cha Taaluma maombi yake hayatakubaliwa.

vii.) Kwa waliosoma nje ya Nchi Elimu ya Kidato cha Nne na kidato cha Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).

viii.) Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.

ix.) Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali

x.) Mwombaji awe ambaye hajawahi kuajiriwa Serikalini.

xi.) Maombi yatapokelewa katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika kipindi cha **siku 14** kuanzia tarehe ya tangazo hili **(12 Juni, 2023)** na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **26 Juni, 2023**

**MAOMBI YA KAZI YATUMWE KWA:-**

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa,
S.L.P 65,
**KILOSA**

Kisena M. Mabuba
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KILOSA**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KILOSA

**Nakala:** Mbao za matangzo,